GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **249** Ramadhan-Shawwal **1446** AH Machi– **2025** Amma **1404** HS BEI TSH 800/=

MWONGOZO WETU KUHUSU MWEZI WA RAMADHANI

Muhtasari wa Hotuba ya Hadhrat Khalifatul masih V a.t.b.a. katika Sala ya Ijumaa ya 3 Juni 2016.

Khalifa Mtukufu alizungumzia juu ya Maswala mbalimbali yahusuyo Ramadhan.

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Inshallah ndani ya siku chache zijazo mwezi wenye baraka wa Ramadhani utaanza.

Pamoja na kwamba katika baadhi ya nchi siku hizi mchana ni mrefu sana na hivyo kufunga saumu kunakuwa kugumu, hata hivyo kufunga saumu ni lazima kwa wale walio wakubwa na ambao wana afya.

Katika nchi ambazo mchana ni mkubwa sana hadi masaa 22 au 23 wafungaji wa nchi hizo wapange muda wao wa kula daku na kufuturu kwa kutumia majira ya nchi za jirani, vinginevyo hakutokuwa na muda wa daku, wala futari, wala muda wa Tahajjud, Sala ya Alfajr au Sala ya Isha.

Kufunga ni moja ya nguzo za msingi za Islam. Kuna baadhi ya maswali yanayoulizwa kuhusu saumu, muda wa kula daku, muda wa kufuturu na hukumu ya kufunga mtu akiwa mgonjwa au safarini. Kwa fadhili za Allah maelfu ya watu wanajiunga na Jumuiya kila mwaka wengine wakitokea madhehebu mbalimbali za Kiislamu na wengine

UK. 03



JAMIA AHMADIYYA WAADHIMISHA MKUTANO WA SEERATUN NABIYY[saw]

Mkutano wa seerat un nabiyy[saw] uliasisiwa na Hazrat Muslih Mau'ud r.a mnamo tarehe 17 june 1928 kwa shabaha ya kutoa hotuba na maelezo fasaha juu ya Maisha, khulka na sera bora kabisa za Mtume Mtukufu[saw] kwa jamii, na kwa njia hii uadui wa Mabaniani, Masingasinga na hata Wakristo ulipungua sana nchini India.



Mwaka huu 2025 katika chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya, mkutano wa Seerat un-nabiyy[saw] ulifanyika siku ya Juma pili ya tarehe 26 January 2025 kuanzia saa nne kamili asubuhi hadi saa saba na robo mchana. Mkutano ulifanyika katika ukumbi wa chuo Kihonda Morogoro. Mgeni rasmi katika mkutano huo alikuwa ni Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib ambae ni Naibu Amir na Principal wa Jamia Ahmadiyya. Mkutano ulianza kwa usomaji wa Qurani tukufu iliyosomwa na bwana Abdurrahman Ramadhani Rundo na kufuatiwa na shairi la kiurdu lililosomwa na bwana Shaddad Said. Baada

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

DAWA YA 'DAJJALI'

Kitabu pekee duniani kinachodai kuwa hakina shaka ndani yake ni Qur'an Tukufu. Ndani ya kitabu hicho tunakumbushwa tuache majivuno na mikogo ya kupandisha mabega. Tunaambiwa walikuwepo matajiri kuliko tulio nao hivi leo. Yalijengwa majengo marefu na ya kifahari kuliko tunayoyaona hivi leo. Wapo waliokuwa na nguvu wakiwatetemesha wengine na wakikohoa tu ardhi ilitetemeka. Hivi leo yamebaki masimulizi na habari zao zimo katika kaburi la sahau.

Hayo yote yameelezwa ili tusianguke katika shimo walimoanguka wenzetu. Lipo taifa hivi leo, likisema sasa hivi ni asubuhi wakati ni usiku inatakiwa sote kwa sauti moja tuitikie tena kwa sauti kubwa 'ndiyo bwana'. Wakisema kule kuna silaha za maangamizi mahali fulani, sote bila uchunguzi au upelelezi wa aina yoyote tunatakiwa kukubali kwani bwana mkubwa hakosei. Majivuno ya bwana mkubwa kwa hivi sasa yamefurutu ada. Ana badili majina yaliyopo. Baadhi ya nchi ameahidi kuzichukua. Hivi karibuni amekuja na wazo linalotonesha donda la kihistoria. Mwaka 1948 Wapalestina walisukumwa kutoka katika ardhi yao na kwa mabavu likaanzishwa taifa la Israil.


Khalifatul Masih[II], Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra] aliendelea kupigania haki za Wapelestina hadi mwisho wa maisha yake. Sir Muhamamd Zafrullah Khan[ra], sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa[as] na Mjumbe wa kudumu wa Pakistani katika Umoja wa Mataifa alitoa hotuba ya kihistoria akilaani dhulma waliyokuwa wanafanyiwa Wapalestina. Mateso ya Wapalestina hayajaisha. Mapatano na mapatano yamefikiwa. Kwa mathalani mapatano ya 'Oslo', mapatano ya 'Abraham' yote hayo yamemwagia petrol kwenye nyumba inayoungua. Nyuma ya mbinu hizi zote ni Dajjali.

Sasa Dajjali amekuja na mpango mpya. Eneo la Ghaza lililoteketezwa sana tena kwa makusudi. Na Dajjali sasa anasema mahali hapo hapafai kwa kuishi. Wapalestina wachukuliwe na Misri na Jordan. Lakini ukweli ni kwamba wanataka mahali hapo pachukuliwe na walowezi wa Kiyahudi. Wazo hili mufilisi limepingwa vikali na pande zote za Dunia.

Na wapalestina wenyewe wamesema ni bora waendelee kuishi kwenye vifusi kuliko kuacha ardhi yao. Hawakukubali na hawajawahi kukubali kuisaliti ardhi yao.
Dini ya Islam, ndiyo yenye dawa ya matatizo yote yanayoikabili dunia kwa hivi sasa. Ni dini ambayo inaweza kuleta Amani na utengamano.

Lazima ikumbukwe ya kwamba hakuna nguvu inayoweza kushinda njama na vitimbwi vya Dajjali isipokuwa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Wale wanaotafuta suluhu ya tatizo la Palestina wakumbuke ya kwamba nguvu pekee ya kupambana na Dajjali ni kwa kupitia Masihi Aliyeahidiwa[as].
Habari njema ni kwamba Masihi Aliyeahidiwa[as] amekwishadhihiri.
Tunao wajibu wa kumpokea ili matatizo haiyo yaweze kutatuliwa.
Masihi Aliyeahidiwa ni Nabii wa Allah na hakuna kheri yoyote katika kumkataa Nabii wa Allah. Mpokeeni Masihi Aliyeahidiwa[as] ambaye ametumwa kusimamisha shani na utukufu wa dini tukufu ya Islam.

Dawa ya kumteketeza Dajjali ni kumpokea Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]. Na kama alivyosisitiza Khalifatul Masihi –V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] katika hotuba yake ya Ijumaa ya tarehe 07/02/2025 Waislam wanatakiwa kuungana. Na muungano wao uwe chini ya bendera ya mwana wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhamamd[saw] yaani Masihi Aliyeahidiwa[as].



QUR'AN TUKUFU

9. Na ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao. *Al-Mu'Minuun 23:09*

وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ۝



NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar r.a. ya kwamba Mtume[saw]. alisema: Kila mmoja wenu ni mchungaji na kila mmoja wenu ataulizwa kuhusu raia wake. Amiri ni mchungaji. Na mtu ni mchungaji wa watu wa nyumbani mwake. Na mwanamke ni mchungaji wa nyumba ya mumewe na watoto wake. Basi kila mmoja ni mchungaji na kila mmoja ataulizwa kuhusu raia wake. (Bukhari)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

Moyo wangu unakuwa hautulii kufikiria kwamba watu hawa ambao wana muelekeo wa njia iliyo nyooka hawajiletei madhara peke yao kutokana na maovu yao wenyewe, badala yake, huwapa wengine fursa ya kuucheka Uislamu pia. Ni kwa sababu hii kwamba katika sensa iliyotangulia, Bw Ibbetson ameandika mengi juu ya Waislamu. Katika hili, nataka kubainisha kwamba Waislamu wanajiita Waislamu lakini wanahusishwa na vitendo vya haramu na haramu ambavyo sio tu vinawatia shaka, bali pia Uislamu. Kwa ufupi, tengeneza tabia na mwenendo wako kwa namna ambayo hata makafiri (ambao kwa hakika wanataka kuukosoa Uislamu) wasiweze kupata kosa kwako.

Mwisho...

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

MWONGOZO WETU KUHUSU MWEZI WA RAMADHANI

Kutoka uk. 01

wakitokea nje ya Islam. Tunao wajibu wa kuwapatia hawa wote majibu muafaka ya maswali hayo ili mioyoni mwao musibaki wasiwasi na wapate utulivu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitumwa akiwa hakimu muadilifu. Alikuwa aje atoe maamuzi ya maswali yote yatakayojitokeza kuhusu misingi ya Islam. Alifafanua haya yote na kutupatia majibu na hivyo ni wajibu wetu kuangalia maamuzi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.katika kila tatizo. Leo nitafafanua kufusu maoni na maamuzi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.juu ya maswali mbalimbali kuhusu saumu na tuelewe kwamba maamuzi yake ndiyo ya mwisho katika zama hizi. Tukumbuke kwamba kanuni nambari moja ya Islam ni taqwa. Hivyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Fungeni kwa uaminifu wote na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Baadhi ya nyakati watoto huuliza kwa nini sisi tunaanza Ramadhani na kufungua tofauti na Waislamu wengine? Hakuna amri hiyo. Hatufanyi hivyo kwa makusudi na wala sio lazima siku zote iwe tofauti. Kuna nyakati ambapo tulikuwa tunafunga na kufungua siku moja. Katika nchi za kiislam au ambazo waislamu ni wengi kwa kawaida kuna kamati za kutangaza kuonekana kwa mwezi baada ya kujiridhisha. Katika nchi kama hizo sisi Waahmadiyya tunafunga na kuadhimisha Idi sawa na matangazo ya kamati hizo. Lakini katika nchi za magharibi hakuna kamati kama hizo wala tangazo rasmi kutoka serikalini, hivyo tunategemea kuonekana kwa mwandamo. Iwapo mahesabu yetu hayakwenda sawa, na mwandamo umeonekana kabla, tunaweza kuanza Ramadhani kabla, iwapo ushahidi umetolewa na mtu mchamungu. Kusema tu tuanze kufunga ili tuende sawa na wasio Waahmadiyya bila kuuona mwezi sio sahihi.

Huzur akasema Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika katika kitabu chake Surma Chasham Arya kuhusu hili: Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakupinga kufanya mahesabu kwa sababu hilo pia ni tawi la sayansi, lakini pia ameonesha umuhimu wa kuuona mwezi kwa uhalisia. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema "Mwenyezi Mungu amejaribu kurahisisha njia za kutekeleza amri kwa kuieleza jamii njia rahisi na za uwazi badala ya kuyafanya mambo kuwa magumu na yenye utata."

Huzur alisema pia kutegemea tu mahesabu ya kamati za kutangaza mwezi kwamba mwandamo utakuwa siku ya 29 au 30 pia sio sahihi. Tunatakiwa tutegemee kuuona mwezi halisi. Pia Huzur alisema, Masihi Aliyeahidiwa a.s.amesema daima tusifuate tu mahesabu au nadharia. Makosa yanaweza kutokea. Ni jambo la wazi kwamba mtu asitegemee moja kwa moja juu ya sayansi bali pia afuate kuonekana kwa mwezi mwandamo. Pia mtu azingatie kwamba siku za kufunga hazizidi 30. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema "Kuuona mwezi ni jambo bora zaidi kuliko mahesabu. Baada ya kufanya uchunguzi wa kutosha juu ya hili, wanaulamaa wengi wa Ulaya wameonelea ni vyema kuushuhudia mwezi mwandamo."

Baadhi ya nyakati kuna uwezekano wa kutokea kosa. Masihi Aliyeahidiwa a.s.aliwahi kukabiliwa na hali hiyo. Rafiki mmoja kutoka Sialkot alimweleza Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba Ramadhani imeanza kwa kuchelewa hapa Qadian kuliko Sialkot ambako mwezi ulikuwa umeonekana kabla. Je tufanye nini maana siku moja itakuwa imepungua. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akajibu itabidi tufunge siku moja baada ya kumalizika kwa Ramadhani.

Kisha kuna swali la kula daku. Ni lazima kula daku kabla ya kufunga. Mtukufu Mtume s.a.w. aliamrisha kufanya hivyo. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema mtu ajitahidi kula daku kwani kuna baraka katika kufanya hivyo. Masihi Aliyeahidiwa a.s.na masahaba zake waliagizwa kula daku na kulikuwa na matayarisho maalum kwa wageni. Hazrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad Sahib r.a. ameandika kwamba Munshi Zafar Ahmad sahib wa Kapoorthala, alimwandikia kumweleza kwamba wakati alipokuwa akitembelea Qadian alikuwa akikaa chumba kilicho jirani na Masjid Mubarak. Siku moja alikuwa akila daku na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akapita karibu yake na kumuuliza unakula daku ya chapati na dengu? Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliwaita waandalizi na kuwauliza je hili ndilo daku ambalo tunawapatia marafiki zetu? Basi akawaagiza waandalizi kwamba wawaulize wale wote wanaofunga, juu ya daku wanalopendelea na matayarisho yafanywe.

Msimamizi aliondoka na kuja na chakula nilichokipenda.

Nilikuwa nimeshakula na adhana ikaanza kusomwa. Masihi Aliyeahidiwa a.s.akaniambia: Usiwe na wasiwasi endelea kula, kwani leo adhana imetolewa mapema.

Kuhusu kusali tahajjud na kula daku pamoja na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Hazrat Mirza Bashir Ahmad Sahib r.a. anasimulia kwamba Dr Mir Muhammad Ismail Sahib r.a alisema mnamo mwaka 1895, nilitumia mwezi wote wa Ramadhani nikiwa Qadian na nikasali Taraweeh au Tahajjud nyuma ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikwua akisali witri nyakati za mwanzoni mwa usiku na baadae kuamka na kusali rakaa 8 za tahajjud katika nyakati za mwisho wa usiku. Alikuwa akisoma Ayatul-Kursi katika Rakaa ya kwanza na Surah Ikhlaas katika rakaa ya pili. Pia alikuwa akisoma Ya Hayyo Ya Qayyum bi rahmatika astaghees kwenye Rukuu na Sujood. Alikuwa akisoma kwa namna ambayo nilikuwa nikimsiakia waziwazi. Kisha alikuwa akila daku baada ya tahajjud na alikuwa akiendelea kula hadi adhana inapomalizika. Hazrat Mirza Bashir Ahmad Sahib r.a. anasema hakuna mahusiano ya moja kwa moja kati ya adhana na kula daku. Hadi pale weupe wa asubuhi utakapoonekana mtu anaruhusiwa kuendelea na daku. Muda wa adhana unahusiana na muda wa sala. Sheria haiagizi kuacha kula kwa kusikia adhana. Wakati mtu wa kawaida anapoona kwamba kumepambazuka hapo ndipo aache kula daku. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema adhana inayotolewa na Bilal isikuzuieni kula daku hadi pale mtakaposikia adhana ya Ibn-e-Maktoum r.a. Ibn-e-Maktoum alikuwa kipofu na alikuwa akitoa adhana tu baada ya kuwasikia watu wakisema kwamba kumekucha.

Mwaka jana nilimweleza rafiki mmoja kwamba alikuwa anakula kwa kuchelewa sana na akaamua kufunga tena. Hakuhitajika kufunga tena iwapo anafuata mawazo ya hapo juu. Katika nchi za magharibi, kwa vile adhana haitolewi kwa sauti, kuna umuhimu wa kuona kwamba kumekucha.

Hazrat Mirza Bashiruddin sahib r.a. alisema kwamba katika mwaka 1903, Dr Khalifa Rashid ud Din sahib na mkewe r.a. walikuja Qadian na kubaki kwa siku nne. Wakaonyesha hamu yao ya kufunga wakiwa Qadian. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akawaletea daku ya chapati za Kashmiri, na akawahudumia yeye mwenyewe. Kisha akasikia adhana na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akawaambia Mwenyezi Mungu anasema katika Quran tukufu: "Na kuleni na kunweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe kutoka katika uzi mweusi wa alfajiri." (2:188) Masihi Aliyeahidiwa a.s. akasema watu hawafuati amri hii na hivyo kuwataka waendee kula wakati adhana inaendelea na pia akasema mwadhini siku

UK. 11

Kwa mwendelezo wa Makala hii piga simu au WhatsApp +255 658 971 662

TANGAZO

UONGOZI WA LAJNA IMAILLAH TANZANIA UNAWATANGAZIA LAJNA NA NASRAT WOTE NCHINI KUWA IJTIMAI YA LAJNA IMAILLAH YA MWAKA 2025 ITAFANYIKA TAREHE 20,21 & 22 YA MWEZI JUNI KATIKA ENEO LETU LA KITONGA JIJINI DAR ES SALAAM.

KILA MWANATANZIMU ANAHIMIZWA KUMALIZA MCHANGO WAKE WA IJTMAI NA KUWEKA NIA YA DHATI YA KUHUDHURIA IJTMAI HIYO PAMOJA NA KUJIANDAA KUSHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KIELIMU NA MICHEZO.

PIA WANATANZIMU WANAKUMBUSHWA KUSHIRIKI SHINDANO LA INSHA PAMOJA NA LILE LA QURAN KWA NJIA YA KUJIREKODI AMBAPO MWISHO WA KUTUMA INSHA NA AUDIO HIZO ZA QURAN KWA WASHIRIKI WOTE NI TAREHE 29/02/2025.

PIA WAJUMBE WOTE WA SHURA KUTOKA MATAWI MBALIMBALI NCHINI WANAKUMBUSHWA KUJIANDAA NA SHURA YA KITAIFA ITAKAYOFANYIKA SIKU YA JUMAPILI YA MWEZI JUNI.

WASALAAM.

QADIAN: Maelezo mafupi na muhimu kwa Jamati Ahmadiyya

Kutoka Uk 12..

Mtume[saw] kudhihiri siku za mwisho baada ya karne nyingi za nuru ya Islam kufifia. Wakati Maka na Madina inabaki kuwa Miji mitakatifu kwa Waahmadiyya kama ilivyo kwa waislam wote, kwa Waahmadiyya Qadian inafuata kwa umuhimu.

Kutoka Qadian. Masih Aliyeahidiwa (as) kwa amri ya Allah alitangaza kuwa ni Masih na Mahdi, Mujadid aliyeteuliwa ambaye ametabiriwa na vitabu vingi, Manabii na dini. Mwenyezi Mungu mwenye uwezo Alimfunulia nakufanya wewe kuwa Isa Mwana wa Mariam na Allah Ana uwezo wa kufanya Anavyotaka(Tadhkirah uk 136). Kumhusu Mahdi, Mtukufu Mtume Muhammad[saw] anasema Itakuwaje hali yenu atakapokuja mwana wa Mariam kutoka miongoni mwenu na atakuwa Imam kutoka miongoni mwenu (Bukhari, Kitabu Anbiya, Bab Nazool Isa).

Masikani yake yakiwa Qadian kwa msaada mkubwa wa Allah, Masih Aliyeahidiwa[as] alifanya kazi aliyopewa na Allah ya kuwaita binadamu waelekee kwa Mola wao. Kazi ambayo maisha yake yote aliifanya ya kuilinda na kuitetea Islam iliyokuwa inashambuliwa kutoka kila pembe na wafuasi wa dini hiyo wakiwa wamekata tamaa, kuipapatikia dunia na kuzama katika maasi. Kutoka Qadian Masih Aliyeahidiwa[as] akaeneza mafundisho sahihi ya Islam na akiwaita binadamu kwenye dini ya kweli. Aliandika zaidi ya vitabu 80-(Msomaji mpendwa, wewe umesoma vingapi?) barua lukuki, Mihadhara isiyo na idadi. Akiona udhalili wa Islam aliomba msaada wa kimbingu. Akimuhakikishia ushindi, Allah alimfunulia siri ambazo hazijulikani ikiwemo siri juu ya ushindi wa Islam, ukweli uliojificha kama kifo cha Isa[as] na kumhakikishia kuwa Islam Ahmadiyya itaenea pembe zote za dunia.

Kudhihiri kwa Masih Aliyeahidiwa katika Qadian ni ushahidi juu ya ukweli wa madai yake. Manabii waliopita na Mujadid walisha tabiri kuwa Mujadid Aliyeahidiwa atadhihiri Kadiani. Kuhusu sehenu atakapodhihiri Masih Aliyeahidiwa, Nabii Isa[as] anasema, kama vile nuru itokavyo mashariki na kun'gaa magharibi na hivyo hivyo ujaji wa mwana wa Adamu(Matayo 24:27). Nabii Isa[as] alikuwa Jerusalem alipotoa bishara hii na Qadian India alipozaliwa Hazrat Ahmad[as] ni mashariki ya Jerusalem.

Hali kadhalika Guru Baba Nanak aliyekuwa mtu wa dini sana na Mcha Mungu ambaye alipata wahyi kutoka kwa Allah alieleza kuwa Mujadid wa dini atadhihiri katika miaka ya 1890, mwisho wa utawala wa Mughal(Jama in Sakhi wa Bhai Bala uk 272) Guru Nanak aliendelea kuthibitisha kuwa Mujadid huyo atakuwa Muislam, Mchamungu na mkweli na atadhihiri karibu na Batala katika wilaya ya Guardaspur Janam sakki uk 234, 231 na 452) Kwa hakika bishara hii inamhusu Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] aliyezaliwa na kuishi Qadian kilomita 18 kutoka Batala. Guru Nanak alizaliwa na kuishi mwaka 1469 na kufariki 1539. Alikuwa ni Kiongozi wa kiroho wa India ambaye aliishi miaka mingi kabla ya kudhihiri kwa Masih Aliyeahidiwa. Guru Nanak anakubalika kuwa muanzilishi wa singa singa.

La kuzingatia ni kwamba Mtukufu Mtume[saw] alitabiri kwamba Mahadi atadhihiri mashariki ya Damascus na huko ndiko iliko Qadian. Mtukufu Mtume[saw] aliendelea kutaja sifa atakazo kuwa nazo Mahadi ambazo zote zinaashiria kwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as]. Hizo ni pamoja na jina lake litafanana na Mtume[saw]. Mtume[saw] anaitwa pia Ahmad ingawaje majina Muhammad na Ahmad yana uhusiano wa aina fulani yakiwa na maana-anayestahili kusifiwa, anayesifiwa.

Mtukufu Mtume[saw] alieleza kuwa Mahdi atatokana na wafarisii na atakuwa na uhusiano na Mtukufu Mtume[saw] na kweli Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wazazi wake ni wafarisii.

Alisema ya kwamba Masih ataanzisha Ukhalifa. Alipokwisha fariki Masih Aliyeahidiwa[saw] mwaka 1908, taasisi ya Ukhalifa ilianza tena. Kwa hivi sasa jumuiya iko chini ya khalifa wa tano Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba] Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alitumwa akiwa Mtume chini ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw].

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] alidhihiri kuwa Masih Aliyeahidiwa sawa na tabiri nyingi zinazopatikana katika dini ya Islam. Yeye ni Mtume mfuasi kama Nabii Isa[as] alivyokuwa kwa Nabii Musa[as]. Mtume[saw] alimwita Isa[as] sawa na majukumu aliyopangiwa kutimiza Isa wa Nazareth.

Alikufa kifo cha kawaida katika uzee huko Kashmir ambako kaburi lake lipo. Ni kazi bure kufikiri kuwa Isa[as] atadhihiri yule yule. Nabii mfuasi ni Nabii ambaye haleti sheria na Yeye huja kuwarejesha watu kwenye njia iliyonyooka njia alimopita Nabii aliyeleta sheria.

Nabii Isa[as] alipodhihiri aliwahakikishia watu ya kwamba hakuja kutengua sheria ya Musa[as] bali kuitimiza (Mathayo 5:17) Kwa mtindo huo huo, Mtukufu Mtume[saw] alieleza kuwa Imam Mahdi[as] atadhihiri miongoni mwa wafuasi wake. Na alisema, atateremka miongoni mwenu waislamu na atakuwa Imam kutokana na nyinyi(Bukhari, Kitabul Anbiya, Bab Nazool Isa). Hivyo atakuwa chini ya sheria ya Kuruani Tukufu na mwenendo wa Mtukufu Mtume[saw]. Wajibu wake itakuwa kuwakumbusha watu ili wafuate njia aliyopita Mtukufu Mtume[saw]. Mtukufu Mtume[saw] alitabiri kuanguka kwa Islam na kuacha mafundisho yake, alisema "Hapana shaka wakati utafika kwa watu ambao kwao Islam itabaki jina tu. Qur'an itasomwa tu kama sehemu ya sherehe na hakuna atakayetekeleza yaliyomo". Bila shaka misikiti itakuwa mingi, lakini haitakuwa chimbuko la nuru na mwongozo. Maulamaa watakuwa wabaya chini ya jua, fitna yote itatoka kwao na adhabu ya Allah itashuka kwenye vichwa vyao(Kanz-al-Ummal juz 6 ukurasa 49).

Aliwapa waaminio tumaini katika zogo na taharuki hiyo atadhihiri Imam Mahad[as] ambaye atawarejesha binadamu kwenye ukweli na kuwatakasa Waislamu na kuwapatia Islam safi. Qadiani ni mji wenye hadhi katika Punjab India. Kitovu cha mapinduzi ya dini duniani. Mapinduzi yaliyoanzishwa na Masih Aliyeahidiwa[as]. Ni hapo ambapo jumuiya ya Ahmadiyya na Ukhalifa vilipoanza chini ya maelekezo ya kimbingu, Masih Aliyeahidiwa[as] alianzisha Jamati mwaka 1889 na sherehe za kwanza za biat zilifanyika Ludhiana tarehe 23 march 1889 na hivyo kuweka msingi jumuiya ya waislamu Ahmadiyya. Hazrat Maulvi Nurudin[ra] alikuwa mtu wa kwanza kuchukua biat kwa mkono wa masih Aliyeahidiwa. Jamati iliyoanza ikiwa ndogo Qadian, sasa imekuwa jamati ya kimataifa na imeenea katika nchi

MATOKEO BAADA YA SHEIKH MBONGO KUONDOKA

Kutoka Uk 12..

hakutosheka na jawabu hilo na alisisitiza kwamba bila ya shaka yupo aliesema muda umekwenda tusalini ni nani ?

Jawabu halikutoka kwamba fulani ndiye aliyesema . Lakini imamu alimtuhumu yule aliyetoa kauli kwamba tuliona muda mrefu umeenda tukaamua tuswali.

Imamu alimpelekea salamu (ujumbe) mtuhumiwa "Haiwi magogo hayakeshi itakuwa chanja?" hio ndio lugha ya Kipemba maana yake ni kwamba watu wakubwa wakubwa hawakuniweza seuze wewe mdogo tu. Utanifanya nini ?Huniwezi ".

Mtuhumiwa alipokea salamu naye akarudisha jawabu akisema. " Kamwambie kama hajaziona chanja zikikesha ataziona mwaka huu. llipomfika jawabu imamu akawa amehakikisha kwamba ndiye yeye alietoa amri ya kuswali na kwamba pamoja na kosa alilolifanya amekuwa na kiburi anathubutu vipi kujibizana na mimi. Basi huo ukawa ndio mwanzo wa mapambano kati ya wawili hao wakitumia silaha zao za jadi ((uramali). Isivyo bahati imamu akawa wa kwanza kuangushwa, alianza na homa kisha ukawa ugonjwa na hatimae kifo. Ugonjwa ulidumu kwa takriban mwaka mmoja.

Hospitali haikutumika muda wote huo kwani mgonjwa aliamini kwamba maradhi yake haya hayawezi kutibika hospitali. Niuramali ni shirki ni uchawi hivyo imamu hakupona alifariki. Hayo ndio matokea ya Imamu aliyeuliza "Mumemuona majani alivyo mfedhehesha mgeni wetu ? Tumfanye nini ? "kibao kilimgeukia akenda na maji. Hii ndio dalili tosha kwamba jumuiya hii ipo kwa amri yake Allah[sw] anaitetea, anailinda na anawasaidia waumini wake.

JAMIA AHMADIYYA WAADHIMISHA MKUTANO WA SEERATUN NABIYY[saw]



ya shairi hilo, ilifuata hotuba ya kwanza yenye maudhui isemayo, "Ibada za Mtume Mtakatifu s.a.w kwa Mwenyezi Mungu." Mada hii ilitolewa na Ismail Abdullatif Pembe. Muhutubu alitoa mifano kadhaa ya kuvutia juu ya namna Mtume mtakatifu[saw] alivyo dumisha ibada ya Allah katika Maisha yake yote. Alisema, kunanyakati ambapo Mtume[saw] alimuomba ruhusa Hazrat Aisha r.a ili atumie muda wa usiku kumuomba Mola wake, hii pia inaonesha jinsi Mtume s.a.w alivyo jali na kuthamini haki za Allah na waja wake. Baada ya hotuba hiyo, ilifuata hotuba yenye maudhui isemayo, "Mabadiliko (mapinduzi) aliyoyaleta Mtume Mtukufu kwa Masahaba wake r.a." Hotuba hii ilitolewa na Mwalimu Shamuni Mwishehe Juma. Katika Hotuba yake Mzungunzaji alinukuu aya ya 128 kutoka katika sura Attaubah, kisha alinukuu tukio la kuharamishwa kwa pombe, kamari n.k na jinsi Masahaba[ra] walivyo tekeleza mafundisho hayo na kujiletea mabadiliko makubwa katika Maisha yao yote.

Baada ya Hotuba hiyo ilifuata Hotuba nyingine iliyochukuwa Maudhui isemayo, "Maisha ya kila siku kwa Mwaminio sawa na Mtume s.a.w au nidhamu ya Maisha kwa Ujumla" mada hii ilitolewa na Maulana Sheikh Aziz Ahmad Shahzad Sahib. Sheikh Sahib alinukuu aya kadha za Qurani Tukufu na maelezo mbali mbali ya Mtume Mtukufu s.a.w juu ya taratibu za Maisha ya kila siku ya mwaminio kuanzia kulalala, kuamka, kukaa, kula n.k Aidha sheikh sahib aliwataka wasikiilizaji kuchukua na kufanyia kazi maelekezo haya ya Mtime s.a.w katika Maisha yao ya kila siku.

Baada ya Hotuba hiyo, zilifuata nasaha chache za Mgeni rasmi Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib Principal Jamia Ahmadiyya na Naib Amir hapa Nchini. Naye alianza kwa kunukuu Aya ya 22 kutoka katika suratul Ahzab inayosema kuwa "Mtume Mtukufu s.a.w ni Mfano mwema wa kuigwa, kisha alimsalia Mtume Mtukufu[saw] na kuanza kwa kueleza kusudio la Hazrat Muslih Mauud r.a Kuanzisha siku hii ili kujua jinsi gani Mtume Mtukufu[saw] alivyoishi na kupata mafanikio katika kila nyanja ili nasi tuweze kufaidika kwayo na kuwafaidisha wanajumuiyya na Jamii kwa





Ujumla. Alimnukuu Hazrat Masih Mau'ud[as] pale aliposema "mafanikio ya kweli hupatikana tu kwa kumfuata Mtume huyu Mtukufu[saw]" Aidha alisema kuwa mafanikio ya Mtume[saw] na mageuzi makubwa aliyoyaleta duniani ni jambo lililo wazi na hata watu wa Magharibi wanafahamu swala hili, kwani yule mwandishi na Mwana Historia Maarufu Aliyeandika Majina ya watu Mia moja walioleta mapinduzi makubwa duniani alimuweka Mtume[saw] katika nafasi ya kwanza.

Mgeni rasmi alieleza mengi na alihitimisha kwa kuwataka wajhudhuriaji kufaidika na maelezo yote yalio tolewa mkutanoni hapo. Mwisho aliongoza maombi ya kimya na kufunga kikao na kisha za Aduhur na Alasiri zilisaliwa kwa Pamoja.

Bustani ya Washairi

SHABAHA YA RAMADHANI

Mola tupe ramadhani, Tukiwa imara siha
Tufungulie midani, Tukaziishi nasaha
Tuimarishe rohoni, Takakidhi zote jiha
Mola tupe ramadhani, Msaada wa shabaha

Na shabaha tuilenge, Saumu ibada tele
Tuviepuke vigenge, Na mambo ya kina sele
Uhusiano tuujenge, Na uzima wa milele
Mola tupe ramadhani, Msaada wa shabaha

Tupe hizo ramadhani, Ziyeyushe ndani zetu
Tukazipate nurani, Zitubariki na utu
Tuzagaze duniani, Tuzivune hasanatu
Mola tupe ramadhani, Msaada wa shabaha

Faragha tulie chozi, lijaze uso muwako
Iume kuchunwa ngozi, Nijisweke mbele zako
Kwa kwikwi na vikohozi, Nikuombe ongezeko
Mola tupe ramadhani, Msaada wa shabaha

Na nijipwekeshe pweke, Ibada za makusudi
Na nijidekeshe deke, Kwa sifa na kuhimidi
Dunia nipige teke, Kwa masiku maadudi
Mola tupe ramadhani, Msaada wa shabaha

Mola timiza shabaha, Tupokee neemazo
Tujihimu na kuhaha, Tuupate msawazo
Ramadhani ni silaha,Yenye kutupa uwezo
Mola tupe ramadhani, Msaada wa shabaha

KOMBE LA AL- KHALIJI

Huree! Huree! Omani, kombe tumelichukua
Pongezi wetu Sultani, michezo kuipanua
Kombe la thamani, Omani imelinyakua

Goli moja kimiani, timu kuinasua
Msaudi katetemeka uwanjani, penalti ikawauwa
Moto ukawaka uwanjani, nyasi zikaungua

Mashujaa wetu wa Omani, ushindi wakauchukua
Waomani tukapata burudani, nyoyo zikatua
Tukajawa furaha na amani, mioyo ikatua

Qabusi wetu wa amani, umetuletea afua
Mola wetu Rahamani, akuongezee satua
Naye waziri mwenye shani, kombe umelichukua

Wasaudi wakachanganyikiwa vichwani, kombe kulivua
Uongozi wako wa thamani, historia itakutambua
Yasowezekana hapo zamani, sasa yamekua

Pongezi Mwenyekiti mhisani, mpira umekuwa
Al-busaidy mshika sukani, mpira kaufufua
Mola akuondolee nuksani, matatizo kuyatatua

Vigelegele hoi hoi na kani, Omani imelitua
Msirudi nyuma asilani, nyavu kuzipasua
Timu ina nguvu jamani, ja chuma cha pua

Hongera kocha wetu mhisani, timu kuichua
Kombe hatuliwachii abadani, nyumbani limetua
Sisemi kwa utani, kweli nimechungua

Mola akipenda mwakani, tena tutalikwapua
Hakika timu yetu Omani, imepiga hatua
Hakika mashujaa wetu vitani, kazi wamelipua

P.O.Box 1840 CODE 111,
Muscat Air Port, Seeb.
Sultanate of Oman

Tahadhari

Upuuzi wavutia, japo uwe na matesho
Watu waukimbilia, bila jali kifwatasho
Maumivu vumilia, hakuna akipatasho
Tahadhari

Rangi wazichubua, juani wapigwa jasho
Ngozi wazibabua, michoro na miapisho
Vitofu wavitoboa, haiwakosi miwasho
Tahadhari

Sajali wajifanyia, makalio mtunisho
Jinsi wazikwangua, wakike mfananisho
Mwisho wanaugua, maradhi yasona mwisho
Tahadhari

Kwanini wajiumiza, upuuzi ufwatisha
Wema utakutuliza, majonzi takuondosha
Urizike ukiweza, majanga kujiondosha
Tahadhari

Dunia unaiwaza, Kila kitu kina mwisho
Tamaa kiendekeza, uzee kupa jutisho
Ulemavu namaradha, Hilo ndilo hitimisho
Tahadhari

Masihi omary stambuli kisagwa

KARIBU MADIHA HAMISI BUNDU

Karibu ulimwenguni, mwana tulikungojea
Metuweka furahani, hofu umetuondoa
Sasa hatupo fumboni, Binti umetujilia
Karibu Binti Madiha, tulikuwa kikungoja

Madiha bini Hamisi, januari mezaliwa
Makoleni kampasi,kituo acho zaliwa
Mwaka waweza uhisi, mbili sita Iikuwa
Karibu Binti Madiha, tulikuwa kikungoja

Nduguzo walisubiri, Kwa miezi walikaa
Unawakaka wawili, miraji WA awalia
Wapili kaka Fadhili, fujo zitampungua
Karibu Binti Madiha, tulikuwa kikungoja

Sasa dada mutwahira, mdogo kajipatia
Kulea so masihara, mgongo kuuandaa
Kujitahidi subira, kumbembeza akilia
Karibu Binti Madiha, tulikuwa kikungoja

Mola wetu wa huruma, hurumie huyu mwana
Akuwe akiwa mwema, dini nayo shikamana
Mlinde na uhosama, husuda wenye kuona
Karibu Binti Madiha, tulikuwa kikungoja

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

RAZAKI

Yeye ndo mgawa riziki, Huruzuku kwa mafungu
Pindi tupatapo dhiki, Na kughubikwa machungu
Tusisahau huyu rafiki, Mtibu yote machungu
Nakushukuru razaki, Mtufaa kila hali

Watupa tustahilicho, So kila kile tombacho
Tugawapo bila choyo, Wongeza kipunguacho
Twaafiki unenayo, Na turadhi upendacho
Nakushuru razaki, Mtufaa kila hali

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721
Email: shunda267@gmail.com

NIGHOFIRIE

Ee Mola wa Rehema, Umeenea,
Milele unauzima, umetimia
Mola wangu wahekima, nakuletea
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Maombi ninayatuma, kuyapokea
Ujana ulinizama, nikapotea
Ukanijali huruma, nakutambua
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Mengi niliyoyasema, wayatambua
Mabaya n ahata mema, unayajua
Nighofiri ni mzima nay a dunia
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Ujana unahasama, unaudhia
Tujiepushe kauma, kuutumia
Mola mwingi wa huruma, ataridhia
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Mola wangu wa heshima, kwako nalia
Uiondoe dhahama, kujinasua
Dunia hii ya uma, inaudhia
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Ninakuomba Karima, kuyapokea
Mola unipe uzima, wa kukujua
Dunia inazahama, kuichukia
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Mola nijalie mema, kuyatumia
Niyatende kwa huruma, nakurudia
Ghofiri hadi kiyama, napendelea
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Karima ninaegama, kusujudia
Nighofirie daima, ninapokaa,
Nikuone muadhama, kunijalia
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Mola wangu kaditama, ninangojea
Unipayo yalo mema, nimenyongea
Naingoja kwa heshima, kunitwalia
Ee Mungu wa Milele nighofirie.

Mtunzi,
Haruna R. Bundala
S.L.P 54
Kiloleni Bombamzinga – Tabora
Tel; 0783251566

WAJINGA
Kufanya watu wajinga, jambo hilo lina mwisho
Wangapi walitusonga, kwa matusi na vitisho?
Wamezama kama nanga, wenye roho ya korosho
Kuibuka hawawezi, wa mzamo wa kuzama.

Mahmood Hamsin Mubiru-(Wamamba)
Kiwalani-Dar es Salaam.

KUTAJWA
Rabi uliyetukuka, naomba hino neema
Siku yangu ikifika, ya dunia kuihama
Nakuomba ya Rabuka, wanikumbuke kwa wema
Nyuma waliobakia, nao wengine wajao

Mahmood Hamsini Mubiru (wa mamba)

QADIAN: Maelezo mafupi na muhimu kwa Jamati Ahmadiyya

...Kutoka Uk. 04

zaidi ya 200 wakiwemo mamilioni ya wafuasi na hii ni katika karne moja na miaka michache. Athari za mwanzilishi wa Jamaat zinaendelea kuonekana duniani chini ya ukhalifa, jamati inajulikana kwa kueneza Islam ya kweli na kueneza Islam kwa njia ya amani. Kwa hakika Jamati Ahmadiyya ni jamati ya kiislam inayokuwa kwa kasi sana na in shaa Allah itaendelea hivyo mpaka kiyama.

Qadian ndiko ilikozaliwa ukhalifa wa kiahmadiyya kama Madina alipoishi Mtukufu Mtume[saw] palivyokuwa chimbuko Khilafatul Rashidun. Sawa na bishara inayopatikana katika Kuruani Tukufu sura ya 24 aya 56 Allah Alimuahidi Masih Aliyeahidiwa[as] ya kwamba Jamaat itashuhudia dhihirisho la pili la Masih Aliyeahidiwa na msaada wa Allah. Allah alimuahidi kuwa dhihirisho hili la pili litadumu hadi siku ya Kiyama. Alipofariki Masih Aliyeahidiwa[as] Al Hajj Maulvi Hakeem Nur-u-din[ra], mfuasi mashuhuri wa Masih Aliyeahidiwa[as] aliteuliwa kuwa khalifa wa kwanza-Qadian ikawa ndio kituo cha kwanza cha khalifatul Masih. Kufuatia kifo cha khalifa wa 1 mwaka 1914 Hazrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra] ambaye pia ni mwana aliyeahidiwa wa Masih Aliyeahidiwa[as] alikuwa Khalifatul Masih II. Alianza Qadian pakiwa ndipo makao makuu ya Jamati hadi mwaka 1947 alipohamia Rabwah Pakistan kutokana na kuanzishwa kwa taifa la kiislam la Pakistan.

Kabla ya kudhihiri kwa Masih Aliyeahidiwa[as] Qadian kilikuwa kijiji kidogo na mbali kutoka miji mikubwa kama Amritsai pasipo na kituo cha reli wala simu.

Hakikuwa kinafahamika nje ya Punjab(jimbo hili limo katika India) kutokana na usuri huu, Masih aliyeahidiwa[as] alitazamiwa na watu wa macho ya dunia sio kwa heshima inayostahili. Masih Aliyeahidiwa[as] alidai kuwa ameteuliwa na Allah kuwa Mujadid aliyeahidiwa na kutoka hapo akaanzisha Jamati Ahmadiyya. Hapo alikebehewa na dola la kiingereza, watu wa India na waislam wa ndani na nje. Hawa watu hawakufahamu maandiko yaliyo katika vitabu vyao, historia na Allah anavyofanya kazi. Waislamu hawakuweza kutafakari juu ya Kurani Tukufu ambayo ni mwongozo wao inayosema, Allah huwachagua mitume Anapopataka kutoka miongoni mwa watu na majini (Kuruani Tukufu 22:76) Dunia ambayo imezama katika mambo ya kidunia tu na wanaojiita wastaarabu hawakuweza kutafakari juu ya historia na vitabu vya dini ambavyo vinaonesha wale wanaokuja kuokoa dunia wanatoka kutoka kwa watu dhalili, wanadharauliwa na wale wanaojiita wastaarabu. Masih Isa mwana wa Mariam[as] alidhihiri miongoni mwa mayahudi ambao sio tu kwamba walimkataa bali walimuweka katika kila aina ya hatari na hata wakajaribu kumuua msalabani. Waislam wanasahau ya kwamba Mtume [saw] muhuri wa Manabii(Kuruani Tukufu 3:145 na rehema kwa ulimwengu) alikuwa ni Yatima. Allah Alimwinua hadi kwenye vilele vya utukufu ambavyo hakuna binaadamu anaweza kuvifikia. Wakasahau kwamba Allah Hatizami mali tuliyo nayo isipokuwa yaliyo ndani ya nyoyo zetu.

Umaarufu wa Masih Aliyeahidiwa[as] ulivyozidi kuenea ndivyo Qadian ilipopata kujulikana na kujichumia sifa, sawa na utamaduni wa siku hizo watu waliitwa majina sawa na walipozaliwa. Masih Aliyeahidiwa[as] alijulikana kama Hazrat Mirza Ghulam Ahmad Qadian ikituonesha kuwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad ni mzaliwa wa Qadian. Kama vile vile Hussein anaitwa Hussein Batala huyu alikuwa miongoni mwa wapinzani wakali wa Masih Aliyeahidiwa[as], wapinzani wasiojua kitu huwaita waahmadiyya-makadiani bila kujua kuwa huo ni mtindo wa watu wa India na kwamba Qadian ni mji kwa hivi sasa. Qadian ni maarufu kwa sababu ni Masih Aliyeahidiwa[as].

Msomaji mpendwa unayefuata ukweli itembelee Qadian, kwa msaada wa Allah roho yako itauona mwanga alioutabiri miaka mingi iliyopita Mtukufu Mtume[saw]. Kwa hivi sasa wasio waahmadiyya, wasomi, waandishi wa Habari wanatembelea Qadian kuhudhuria Jalsa Salana wakiwa na nia na dhamira ya kufanya utafiti.



Umuhimu na Baraka za Ramadhan

Na Sheikh Karim Ud Din Shams

"Enyi mlioamini mmefaradhishiwa kufunga Saumu kama walivyo faradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allah" (2:183)

Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa tisa sawa na kalenda ya Kiislam. Ramadhani ni neno la kiarabu ambalo kitenzi chake ni ramadha na neno la ramadha linatumika kwa ajili ya joto la jua hivyo maana ya Ramadhani ni joto mbili ambazo huzalika mwilini mwa mwislam yaani joto kwa ajili ya kutekeleza maamrisho ya Allah Mtukufu kisha anajizuia kula na kunywa na kuvumilia juu ya mahitaji yote mengine ya mwili wake. Wale watu wanaosema kuwa kwa sababu mwezi huu unakuja wakati wa msimu wa joto ndio maana huitwa Ramadhan, hawako sahih.

Mwezi wa Ramadhani huitwa Ramadhan kwa sababu huunguza madhambi, kitenzi cha neno Ramadhan ni "Ramadha" ambalo linamaanisha joto kali, kwa kuwa mfunga saumu ya Ramadhani hujisikia shida na taabu ya kiu na njaa, basi huitwa Ramadhan. (Lisanul Arab)

Wanalugha wengine pia wanafikiana kuwa Ramadhani huitwa Ramadhani kwa sababu madhambi yanafutwa humo hivyo imeandikwa kwamba:

(Al-Qamusul Muhiit,J 2 UK 330)

Yaani huunguzwa na kufutwa madhambi kwa wingi kutokana na rehema na msamaha ma'alum wa Mwenyezi Mungu ndani ya mwezi huu.

Safari moja Mtume Mtukufu[saw] alipoulizwa kuhusu Ramadhani basi alijibu kwamba:

"***Mwenyezi Mungu hufuta na kusamehe madhambi ya Waaminio humo***". (Kashful Israr....Allama Mubiidi, Abul Fazal Rashid Uddin,J.1.UK.495)

Imamu wa zama hizi, Seyyedna Ahmad[as] anasema akieleza neno la Ramadha kwamba;

"Joto la jua linaitwa Ramadha, kwa kuwa mtu huvumilia juu ya vyakula, vinywaji na ladha zake zote za mwili kisha huzalisha jazba na joto ndani mwake kwa ajili ya kutekeleza maamrisho yake Allah Mtukufu, joto la mwilini na jazba ya kiroho kuwa pamoja yanakuwa Ramadhani (joto mbili). Wanalugha wanaosema hivi kuwa, huitwa Ramadhani kwani unakuja katika msimu wa joto, si sahih mbele yangu kwa sababu hii haiwezi kuwa sifa kwa ajili ya Waarabu. Maana ya kiroho ya ramadha ni jazba na ladha ya kiroho na msukumo wa dini. Ramadha pia ni joto ambalo mawe na kadhalika yapata kuchemka kwalo."(Al-Hakam,24 Julai 1901).

Inaendelea...

Makala hii inapatikana katika Jaliza hapo liitwalo "***Darsa la Mwezi mtukufu wa Ramadhani 2020***"

JIFUNZE KUPIKA KEKI YA NUSU KILO

Vinavyohitajika

- Siagi ya baking 250g – robo kilo.
- Sukari 250g – robo kilo.
- Unga wa ngano 500g –nusu kilo.
- vanilla kijiko 1 cha kulia chakula.
- Baking powder kijiko 1 cha kulia
- Mayai 6-8

JINSI YA KUTAYARISHA

- Weka siagi ndani ya bakuli la kuchanganyia pamoja na sukari uichanganye pamoja mpaka



vichanganyike vizuri (unaweza kuisaga sukari yako ukitaka lakini si lazima).

- Ikichanganyika vizuri weka yai moja moja uchanganye pamoja pia ichanganyike vizuri.

- anza kuweka unga kwenye mchanganyiko wako Hakikisha unaweka unga wako kidogo kidogo alafu unachanganya na sio wote kwa wakati mmoja.

.weka vanila kijiko kimoja na uchanganye kidogo

. weka baking poda yako na uchanganye
Baada ya hapo mchanganyiko wako utakua tayari kwa kuokwa..

ZINGATIA
Unaweza kutumia mashine ya kusagia keki na kama huna tumia mwiko tu kwa kuchanganyia na itakuwa nzuri tu usikhofu.

Buriani Mzee Rashid Salum Mkono

Na. Mwl. Adam Msekwa



Mzee Rashid Salum Mkono wa Kilosa amefariki usiku wa tarehe 16 Februari 2025 na kuzikwa siku hiyo hiyo ya tarehe 16 saa kumi jioni huko kwao Kilosa Morogoro.
Inna lillah wainna ilaih rajiun.

Mzee Rashid Mkono ni mmoja wa wanajumuiya wakongwe katika wilaya ya Kilosa.

Enzi za uhai wake alijitahidi sana kuhubiri Islam Ahmadiyya na kwa msaada wa Allah matawi kadhaa yalianzishwa enzi za uhai wake.

Mzee Rashid Mkono alikuwa mshiriki mkubwa wa mikutano ya Jalsa salana, ijtimaa nk. Pia alikuwa akipenda sana ukhalifa.

Kwa hakika tumepoteza mtu imara sana katika kuitumikia dini ya Islam.

Allah amjalie msamaha wake na ampe pepo ya juu.
Amen.

Bila ya Khalifa waislamu wataendelea kufanya dhulma hivi hivi

Nimepiga hisabu kama familia moja tu katika nchi moja Saudia Familia ya kifalme wakitoa zaka ya halali juu ya mali zao ambayo ni trillioni 2 Dola.

Kila mtanzania (watanzania wapo 50 miloni) atapata dola 16000 kila mwaka ambayo ni millioni tatu na hela kila mwezi 2.5÷2000000000000 =16000=50000000÷800000000000usd×36000000=2250 tsh

.kila mtanzania anaweza kupata millioni 36 kila mwaka

Sasa hii hisabu ni ya familia moja ya wafalme katika nchi moja tu

Malaki na malaki familia zipo katika saudia na hela ya kutupa Nenda nchi 22 zingine .wengi wao wanao mafuta kama maji...

Wakitoa zaka ya haki wanalisha dunia yote na wanaishi na raha kabisa...

Lakini kwa hakika kinachofanyika ni hela yote inaenda katika vita na kukufurisha watu kununua mabomba na hasa katika ufasiki na zina n.k

Waislamu wanaoishi uarabuni tu wakitoa zaka kihalali na wasaidie watu bila ya kuangalia rangi wala dini dunia yote ingelishwa na hao hao...

Lakini cha ajabu ikitokea ukame au tetemeko nchi yoyote n.k wanaotangulia kuwasaidia ni wazungu ambao hawatoi zaka...lakini wanajitolea hata kuwaonyesha watu lakini wanajitolea ...

Islamu ingekubali na ukhalifa ulioanzishwa na Allah chini ya himaya ya Imam Mahdi Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad AS Islamu ingewabeba watu wote kama ilikuwa juu yao

انتم خير امة اخرجت للناس..

Lakini wanapokataa wataona adhabu siku moja kama Mtume Muhammad SAW alituambia

ويل للعرب ويل للعرب --

MATUKIO KATIKA PICHA



Picha 4 za kwanza ni Tukio la uzinduzi wa Msikiti wa Jamia Ahmadiyya (Masjid Masroor) baada ya kufanyiwa ukarabati, lililokwenda sambamba na maadhimizo ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa (2025) hapo Jamia.



Ziara ya Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Morogoro (Maulana Sh. Abid M. Bhatii Sahib) na Mbashiri wa Mkoa wa Morogoro wakati walipomtembelea Mhe Afisa wa Uhamiaji Mkoa ofisini kwake.



Katika kuadhimisha siku ya mwana aliyeahidiwa Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania iliweza kutembelea shule ya Sekondari ya Ikwiriri na kuwasilisha kile walichojaaliwa kwa ajili ya kuwatia moyo vijana wanaoendelea na safari yao ya masomo katika shule hiyo.

Maswali kutoka katika kitabu cha

MHISANI KWA UBINADAMU

Imetayarishwa na.
Sheikh Ali Dino Tahir - Simiyu

118. Toa Tafsiri ya Sura Al-faatir aya 25. وان من امة الا خلا فيها نذير WA IMMIN UMMATIN ILLA KHALA FIHAA NAZIIR?
Jibu: Hakuna kaumu yoyote ile ambamo hakupita humo nabii.
Uk. 86 119. Kuzibughudhi dini zingine na kuzikataa moja kwa moja,inasihi?
Jibu: Hapana kabisa kwa sababu itakuwa ni kuikataa Fadhili ya Mwenyezi Mungu ambayo haichagui watu fulani.

120. Hisani ya saba ya Mtume iliyoandikwa katika kitabu cha Mhisani… ni ipi?
Jibu: Mtume[saw] alitufundisha kwamba tuwe na adabu kwa watakatifu wa kila kaumu;kwa njia hii tutaishi na amani.

121. Tuseme nini tukimsikia mtu akidai kwamba aliwahi kuja Mja wa Mungu au mtume fulani katika Amerika au Afrika
Jibu:Tunatakiwa tuseme kwamba unachosema ni sawa tu kwa sababu Quran inasema, "alipita mwongozi katika kila kaumu"
Uk. 87
122.Kwanini waislamu wamezuiwa kutaja viongozi au miungu ya wasio waislamu kwa ubaya
Jibu: Kwa sababu wasio waislamu watajisikia vibaya na kutukana Mwenyezi Mungu.
Uk. 88
123. Je, inasihi ,tukisema dini ya Mayahudi au Wakristo au dini ya kibaniani hawana heri ndani yake?
Jibu: Quran tukufu imekataza mambo haya bali Quran inasisitiza kukubali mambo mazuri ya dini zingine na kuzisifu.
Uk. 89,90
124. Wakristo walipokuja kujadilana naye Mtume Muhammad SAW aliwakaribishaje?
Jibu: Aliwakaribisha msikitini, wakaendelea kuongea; ilipofika wakati wa sala zao, walitaka kutoka, Mtume SAW aliwaambia "Fanyeni ibada zenu humu humu." Na wakasali yao katika Masjid Nabawi.
Uk. 91
125. Tunatakiwa kufanya nini wakati vita vinaendelea na maadui wakiona watashindwa na kuomba vita visiendelee.
Jibu: Waislamu wanatakiwa waache kupigana pale pale na haturuhusiwi kabisa kutumia fursa hii kuwamaliza.

126. Ni nini mzizi wa maendeleo ya elimu? Jibu: Mzizi wa maendeleo ya elimu ni uhuru wa Mawazo
Uk. 91,92 127. Ni nini tafsiri ya Surat Albakara aya 257. لا اكراه فى الدين قدتبين الرشد من الغى LAIKRAHA FIDDIN KATTABAYYANA RRUSHDU MINAL GHAYYI.
Jibu: Haipaswi kuwepo na kulazimishana katika mambo ya dini kwa sababu Mungu ameshabainisha tofauti kati ya mwongozo na upotofu.

Uk. 93
128.Toa Tafsiri ya Sura Albaqara aya 229 WALA HUNNA MITHLULADHI 'ALAIHINNA?
Jibu: WANAWAKE NAO WANA HAKI KAMA ZILE WALIZO NAZO WANAUME.

129. Taja jina la Mtu wa kwanza aliyestawisha haki za wanawake na aliweka hisa ya mali kutoka kwa ndugu zake (Wazazi na mume wake)
Jibu: Mtume Muhammad SAW

Uk. 94
130. Je, Mvua huwa inanyesha kwa sababu ya nyota fulani au kwa agizo la Mungu Mtukufu?
Jibu: Mara zote mvua inanyesha kwa agizo la Mwenyezi Mungu.
Uk. 95
131.Mwanyae Mtume SAW Hadhrat Ibrahim Radhiallahu anhu alipofariki siku ile Jua lilpatwa,Masahaba walifikiria kwamba jua lilipatwa kwa sababu ya kufariki kwa mtoto wa Mtume SAW,Mtume alisemaje juu ya hilo ?
Jibu: Mtume alisema kwamba Jua na Mwezi hupatwa kwa sababu ya kanuni fulani ya maumbile ya Mwenyezi Mungu,haina uhusiano wa mauti au uhai wa mtu yeyote.

132. Katika Islam Ni nani hupaswa kutoa Zaka ? Jibu: Kila tajiri aliyefikia au kupita kiwango maalum cha mali yake anapaswa kutoa zaka.

133. Ni nini kiwango cha zaka Jibu: 1. Kwa mfugaji akiwa na mbuzi au kondoo 40 na upite mwaka wasipungue anapaswa atoe mbuzi au kondoo mmoja kwa ajili ya zaka,hivyo wakiwa 80 mbuzi wawili n.k 2 Akiwa anamiliki Ngombe 30 juu ya kila ngombe 30 atatoa Ngombe mmoja . 3. Akiwa ana Ngamia 5 basi mbuzi mmoja.
4. Na ikiwa gramu 483.88 ya Fedha(Silver) au mali inayofanana na bei ya kiasi hicho cha Fedha ikiendelea kuhifadhiwa hadi mwaka mzima basi sehemu ya arobaini itatolwa katika zaka (kwa mfano ukiwa million kumi utatoa laki mbili na elfu Hamsini mara moja katika mwaka)

Uk. 95,96
134. Kwa sababu gani kila muislamu tajiri anaagizwa na Mungu kwamba atoe zaka kila mwaka
Jibu: Ili zaka hiyo wapewe masikini ambao hujituma kwa ajili ya matajiri,na wapewe wasiojiweza na walemavu n.k

135. Ni nani anawajibika kukusanya zaka na kuwapa masikini Jibu: Khalifa au Serikali.

136. Hisani ya 12 iliyoandikwa katika Kitabu cha Muhisani ni hisani gani?
Jibu: Hisani ya 12 ni alipiga kabisa marufuku pombe.
Uk. 97
137. Mtume Muhammad SAW alijitolea kwa ajili ya nini?
Jibu: Mtume SAW alijitolea kwa ridhaa ya Allah Mtukufu na kwa jili ya manufaa ya watu,sio kwa ajili ya faida yake
Uk. 98
138. Kamilisha sentensi ifuatayo: Kazi njema ni zile zenye…..
Jibu: Kazi njema ni zile zenye kudumu ,Hivyo daima muanzapo wema basi jaribuni kudumu nao daima.

Uk. 99
139.Nini maana ya kurbani? Jibu: Kujitolea
Uk. 100
140.Mtume Muhammad SAW alifanya kurbani ya muda gani? Jibu: Mtume Muhammad SAW alifanya kurbani kwa ajii ya ukweli wa kudumu na kwa ajili ya maendeleo ya kudumu.

Uk. 101
141.Nini maana ya kurbani ya matamanio? Jibu: Kuyafuta matamanio kwa ajili ya Allah Mtukufu

142. Nini maana ya kurbani ya Jazba?
Jibu: kuziondoa na kuacha jazba kwa ajili ya Allah Mtukufu

143.Qurbani ya ndugu na jamaa ni nini? Jibu: Kujitenga nao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu

144. Kurbani ya heshima ni nini? Jibu: kuvumilia fedheha kwa ajili ya Allah au kuachana na fursa ya kuheshimika
Uk. 102
145. Aina ngapi za kurbani au aina ngapi za kujitolea zimeandikwa ktk Kitabu cha Muhisani? Jibu: zisizopungua 13

146.Toa mfano wa kurbani ya matamanio aliyofanya Mtume Muhammad SAW?
Jibu: Alimuoa mwanamke mwenye miaka 40 katika ujana wake.
Uk. 103
147.Utuambie sababu angalau moja kwanini Mtume Muhammad SAW alioa mke mwenye umri mkubwa wakati yeye alikuwa kijana?
Jibu: Ili yule mke asipoteze muda wake na yeye apate wakati zaidi wa kuwahudumia viumbe wa Mungu

Uk. 104
148.Ni nani aliyekuwa akimfikishia Mtume Muhammad SAW habari za njama za makafiri wakifanya huko Makka? Jibu: Hadhrat Abbas RA.

149. Hadhrat Abbas alipokuwa anafikishia Mtume habari za njama za makafiri, Je, wakati ule alikuwa muislamu?
Jibu: Hapana, bali alisilimu baadae

Uk. 105
150. Kwanini Mtume Muhammad SAW alikuwa anataka Kamba za mateka wote zilegezwe?
Jibu: Miongoni mwa wafungwa wa Badri mmoja alikuwa Hadhrat Abbas. Masahaba wa Mtume saw walilegeza kamba ya Hadhrat Abbas aliyekuwa anagugumia; Mtume[saw] hakutaka utokee upendeleo fulani kwa sababu ya udugu wake na alitaka uadilifu ufanyike na kamba za wafungwa wote zilegezwe.
Uk. 106
151. Wakuuu wa Makka walipomtishia Hadhrat Abu Talib na kumuambia amzuie Muhammad saw na Hadhrat AbuTalib alipomuuliza kwamba JE HAIWEZEKANI HIVI KWAMBA UACHE KUTOA MAWAIDHA DHIDI YA MASANAMU ILI TUSALIMIKE NA UPINZANI WAO alipoulizwa Mtume alijibu nini? Jibu: Mimi naweza kubeba kila aina ya shida kwa ajili yako, lakini hii haiwezekani kwamba mimi niache kutoa mawaidha ya Umoja wa Mungu na kuupinga ushirikina. Hivyo farakana nami na uniache mwenyewe na hali yangu.
Uk. 107
152. Mtume[saw] alipokataa kukubali sharti za wakuu wa Makka, Je Abu Talib alimuacha peke yake?
Jibu: Hapana bali alimuambia "Ewe mwana wa ndugu yangu, chochote ukisemacho ni cha ukweli nenda na ufanye kazi yako, mimi na jamaa zangu tu Pamoja nawe."
Uk. 108
153. Bintiye Mtume[saw] Bi Fatima alipomjia na kusema "Mikono yangu imetoa malengelenge kutokana na kufanya sana kazi za mikono. Nina Watoto wadogo basi unipatie kijakazi," Mtume alipomsikia alimjibu nini?
Jibu: Malengelenge hayo ni bora kuliko mali zile unazozitaka nikupe.

154. Kwanini Mtume saw hakumpatia kijakazi kumsaidia bintiye Fatima hali alikuwa na haki katika mali hiyo ?
Jibu:Kwa sababu aliona kwa wakati ule mahitajio ya waislamu ni mengi sana kuliko yeye au ndugu yake.

Uk. 109,
155. Hadhrat Abu Janadal Radhiallah anhu alikuwa nani ?
Jibu: Ni Sahaba mmoja aliyesilimu huko Makka wakati Waislamu walikuwa Madina na aliposilimu aliteswa sana na makafiri alipopata fursa akatoroka na kufika mahali paitwapo Hudhaibia wakati huo mkataba wa hudaibia ulikuwa unaandikwa.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

MWONGOZO WETU KUHUSU MWEZI WA RAMADHANI

Kutoka uk. 03

hiyo aliadhini mapema.

Mtu anaweza kutumia chakula kizuri lakini kwa kiasi na mizania. Allah anasema katika Quran tukufu: "Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito ." (2:186)

Saumu imelazimishwa ili kuyarahisisha maisha ya mwaminio na kumwepusha na shida. Lakini baadhi ya watu wanaofikiria kwamba wanashinda na njaa mwezi wa Ramadhani, kwa hakika wanazitusi amri za Quran tukufu. Chakula hasa ni chakula cha kiroho, ambacho kinazirutubisha roho badala ya chakula cha kimwili kinachourutubisha mwili tu. Mtu anatakiwa ajitambue kwamba anafunga na hivyo ale kwa kiasi. Baadhi ya watu huishia kuongezeka uzito badala ya kupungua wakati wa ramadhani. Kwa baadhi ya watu mawazo yote yanakuwa ni kujaza matumbo yao tu badala ya saumu. Wanajilia tu vyakula vya mafuta mengi na tamtam kupita kiasi. Jambo hili hupunguza baraka za ramadhan. Kuna amri ya kuwahi kufuutru na kula daku na hayo ndio yenye baraka. Mtu anatakiwa kula chakula kizuri lakini kwa kiasi. Kufunga katika hali ya ugonjwa na safari kumekatazwa. Mirza Yaqub Baig Sahib anasema alikuja Qadian kutokea safarini wakati wa Alasiri na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamwambia afungue saumu. Pia alipoulizwa kuhusu ugonjwa alijibu, tunaamini kwamba ni lazima kujipatia faida ya ruhusa hiyo. Wale wasemao kwamba msafiri akiweza kufunga, afunge, Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema siioni kauli hiyo kuwa sahihi. Mohayyud din Ibn Arabi hakuona kuwa sawa kwa mtu kufunga akiwa safarini au mgonjwa, na alisema mtu anatakiwa kuzifunga tena siku hizo baadae. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akiwaruhusu wageni kufunga iwapo wanabakia Qadian. Alikuwa hawaruhusu kufunga siku wanayosafiri. Wakati jalsa ilipoangukia ramadhani, wageni walikuwa akipatiwa daku. Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakuwaruhusu watu kufunga wakiwa safarini lakini aliwaruhusu kufunga wale waliokuwa wakitembelea Qadian mara kwa mara na kukaa huko. Iwapo mtu anapanga kukaa sehemu fulani kwa zaidi ya siku 3 anatakiwa kufunga, lakini iwapo atakaa chini ya siku 3 anasamehewa.

Wakati Sheikh Muhammad Chaito alipotembelea Qadian, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alimuuliza iwapo alikuwa amefunga. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamwambia kwa vile alikuwa safarini na pia alikuwa mzee basi afungue saumu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akasema kutii tahafifu zilizotolewa na Quran pia ni sehemu ya uchamungu.

Kuhusiana na Msafiri au mgonjwa kufunga saumu, Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema ni kosa kufunga wakati mtu yu mgonjwa au yumo safarini. Kiini cha utawa ni kutii amri za Mwenyezi Mungu sio mtu kujipangia taratibu yeye mwenyewe. Hakuna utata, maagizo yapo wazi: "Hakuna kufunga wakati mtu yumo safarini au yu mgonjwa". Wakati mgeni huyu Baba Chaito ambaye hakuwa Ahmadiyya alipouliza je iwapo hakuna shida yoyote katika safari kwa nini mtu asifunge? Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamjibu hayo ni maoni yako mwenyewe.

Quran tukufu inasema "Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine" (2:185)

Quran tukufu haijafafanua ni safari ipi au ugonjwa upi. Pia mtu ashike njia inayoongoza kwenye taqwa.

Hazrat Maulvi Noor ud din r.a. alisema kwamba Ibn Arabi alisema kufunga baadae ni lazima hata kama mtu alifunga wakati akiwa safarini au mgonjwa. Kwani Mwenyezi Mungu amesema fungani siku za baadae muwapo wagonjwa au safarini. Hakuna maagizo kwamba utakapofunga ukiwa mgonjwa basi usifunge baadae. Yule anayefunga wakati yu mgonjwa basi anaasi amri ya Mwenyezi Mungu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema kwamba kama vile Mwenyezi Mungu alivyoamrisha kufunga saumu, pia ameamrisha kutokufunga katika mazingira fulani. Mtu anayefunga wakati yumo safarini au mgonjwa anatakiwa kufunga tena wakati atakapopata afya au safari yake kumalizika. Ni lazima kufuata amri hii ya Mwenyezi Mungu. Uokovu hupatikana kwa rehema ya Mungu na sio kwa kulazimisha. Mwenyezi Mungu hajafafanua kwamba mtu awe na ugonjaw mkubwa au mdogo au safari iwe fupi au ndefu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akiwaeleza watu wafungue saumu zao iwapo walikuwa safarini. Alikuwa akisema, wakati Mwenyezi Mungu ameagiza msifunge muwapo safarini basi haifai kufunga. Wakati fulani ukiwa umebakia muda mfupi tu kabla ya muda wa futari, ilikuwa baada ya sala ya Alasiri Masihi Aliyeahidiwa a.s. alimwambia mgeni wake mmoja aliyekuwa msafiri afungue saumu. Mgeni akasema mbona muda uliobaki ni mfupi tu, lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s.akasema huwezi kumfurahisha Mwenyezi Mungu kwa kumlazimisha akubali saumu zako, bali kwa hakika Mwenyezi Mungu anakuwa radhi kwa sababu ya utii wako.

Katika ramadhani mojawapo, Masihi Aliyeahidiwa a.s.alitembelea Amristar. wakati akitoa hotuba bwana mmoja akampelekea chai, lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. akakataa. Yule bwana aliposisitiza sana Masihi Aliyeahidiwa a.s. akachukua kikombe na kunywa kidogo. Wapinzani wakaanza kumtusi kwamba haiheshimu saumu. Baadhi wakamrushi mawe. Sheikh mmoja asiye Ahmadiyya akaleta kebehi kwa kusema: '"Leo watu wamemfanya Mirza kuwa mtume."

Kwa vile Mufti Fazl ur Rehman sahib ndiye aliyempatia chai Masihi Aliyeahidiwa a.s., watu wote walimchukia na wakaanza kumlaumu kwa tukio hilo. Wakati Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipoelezwa juu ya tukio hilo akasema hakufanya kosa lolote kwa kumpatia chai.

Wakati mmoja Masihi Aliyeahidiwa a.s. akiwa Ludhiana alikuwa amefunga na akaugua ghafla hadi kukuaribia kuzimia, hapo hapo akafungua saumu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akipendelea njia iliyo rahisi kati ya ruhusa mbili. Hadhrat bibi Aisha anasimulia hayo hayo kumhusu Mtukufu Mtume s.a.w. Baadhi ya nyakati Ramadhani inakuja wakati wa mavuno. Ni kipindi cha kazi ngumu kwa wakulima. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema matendo hulipwa kutokana na nia. Kila mtu anaweza kujitathimini mwenyewe juu ya msingi wa taqwa. Iwapo mtu atakosa mfanyakazi wa kumvunia, anaweza kukatisha saumu na kufunga baadae. Kwa wakati huo yeye atahesabiwa kuwa mongoni mwa wale wasioweza kufunga.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema, wakati fulani alianza kufikiria kwa nini kutoa Fidya ni lazima. Akasema ni kwa ajili ya kupata nguvu. Mtu anatoa Fidya ili apate nguvu kwani hili laweza kutokea kwa msaada wa Mwenyezi Mungu tu. Iwapo Mungu anapenda anaweza kumpatia nguvu hata mtu dhaifu. Mtu aombe kwa uchungu kwamba O Mola, huu ni mwezi wako ulioubariki, nami najisikia kupungukiwa kwa kushindwa kufunga na pia sina uhakika iwapo nitafika saumu ya mwaka ujao, au kwamba nitakuwa hai... Iwapo mtu ataomba kwa uaminifu, Mwenyezi Mungu ataupa nguvu moyo wake.

Fidya sio mbadala wa kufunga. Fidya ipo ya aina mbili. Ya muda mfupi na ya kudumu. Ya muda mfupi ni kwa wale wanaoweza kuja kufunga na ya kudumu ni kwa wale ambao hawana tena uwezo wa kufunga. Kima cha fidya ni chakula cha mtu mmoja. Kama Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakuweza kufunga alikuwa akitoa fidia na kufunga baadae. Kama mtu hawezi kufunga anaweza kumlisha maskini yeye mwenyewe au anaweza kuchangia kwenye mfuko wa mayatima huko Qadian.

Kama mtu atakula kwa kusahau hakuna adhabu bali anatakiwa aendelee kufunga. Watoto hawaruhusiwi kufunga kwa mujibu wa sharia. Wanaruhusiwa kufunga wanapokaribia umri wa kubaleghe. Mtu hatakiwi kuwafungisha watoto kwani ni kosa. Katika umri wa miaka 12 hadi 13 mtu awazoeshe watoto kufunga siku chache na ifikapo umri wa miaka 18 ndio mtu afunge kwa kudumu. Ni wajibu wa wazazi kuwazuia watoto wasifunge. Baadae watoto wakikua ndipo wazazi wawahimize kufunga. Umri wa miaka 18 umewekwa tu lakini katika maumbile ya baadhi ya watoto wanaweza wasiweze kufunga hadi miaka 21 sawa na hali yao ya kiafya. Binti mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa hapendi watoto wafunge kwa kudumu na baadhi ya nyakati alikuwa akimlazimisha kufungua kwa vile alikuwa mdogo.

Kuhusiana na Taraweeh: Ni ipi hukumu ya kusali rakaa 20. Sawa na sunna ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni bora kusali rakaa 8 kwenye sehemu ya mwisho wa usiku, lakini pia inaweza kusaliwa mwanzoni mwake. Rakaa 20 na zaidi zilianzishwa baada ya mtukufu Mtume s.a.w.. Sunna ya Mtukufu Mtume s.a.w. ilikuwa ni kusali rakaa 8. Kama mtu yumo safarini anaweza kusali tarawehe peke yake. Kwa hakika Taraweeh ndio sala ya Tahajjud.

Mwenyezi Mungu atuwezeshe

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi Ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa

UK. 03

Lajna Imaillah






Buriani Mzee Rashid Salum Mkono

Uk.08

MATOKEO BAADA YA SHEIKH MBONGO KUONDOKA

Na. Ali Hamisi Juma Sahib



Sheikh Mbongo ambaye alikuwa amealikwa kuja kutoa daawa aliondoka. Viongozi waliomleta sheikh Mbongo pamoja na imamu wa msikiti walihuzunika na kitendo kile kilichotokea msikitini, walitafsiri ni udhalilishaji. Wao waliona mimi nimemdhalilisha mgeni wao ila mgeni wao ndiye aliye mdhalilisha Sayidna Ahmad[as].

Imamu wa msikiti alitembelea nyumba hadi nyumba akiuliza. Mumemuona Ali alivyomdhalilisha mgeni wetu ?Tumfanye nini ?" Bila ya shaka imamu huyu alikuwa na dhamira mbaya dhidi yangu ila mimi sikuwa na hofu yoyote ile nikijua kwamba nilichokifanya ni haki pasi na shaka yoyote. Kilichotokea kwanza kabisa. Vijana waliuhama msikiti wakawa wanaswali kwenye msikiti mdogo sana uliojengwa bondeni kwa ajili ya wasafiri na wenye dharura. Fitna hii haikuishia hapo kwa vijana tu iliendelea hadi kwa wazee, siku moja imamu alichelewa kufika msikitini alipofika sala inaendelea ikabidi akae nyuma, jambo hili lilimuudhi sana na baada ya sala aliuliza " Nani alietoa amri ya kuswali ? "

likatolewa jawabu kwamba sisi tuliona muda umeenda ndipo tukaona ni vyema kuswali . I m a m u

HABARI UK> 04

QADIAN: Maelezo mafupi na muhimu kwa Jamati Ahmadiyya

Kutoka toleo lililopita

Na. Mwl. Saleh Yassin



Watu wana sehemu wanazoziheshimu sana na watu wanaowapenda. Waislam duniani kote wanapenda Makka na Madina na wanampenda Mtukufu Mtume[saw]. Wakristo wanaye Yesu[as]. Mabudda wanaye Budda na wahindu wanaye Krishna.

Pamoja na Maka na Madina waislamu Ahmadiyya wanayo Qadian na Masih Aliyeahidiwa, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Qadian ndiyo dira ya kuiongoza Islam katika Imani na mapenzi, mahali ambapo nuru inaangaza pote. Nuru ya mahali hapa patakatifu imeenea sehemu zote za dunia ikizipatia nuru nyoyo zisokuwa na idadi. Sababu ya nuru hiyo ni Masih Aliyeahidiwa[as]. Alizaliwa mwaka 1835 na aliishi hapana kutoka hapa akaeneza nuru duniani kote akifafanua mafundisho ya Islam ya kweli. Masih Aliyeahidiwa aliyedhihiri Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] alitabiriwa na M t u k u f u

HABARI UK> 04



Je, Wajua?

Jonny Kim ni Luteni Kamanda wa Jeshi la Wanamaji la Marekani, aliyekuwa Navy SEAL, daktari (M.D. kutoka Shule ya Matibabu ya Harvard), naval aviator, na astronaut wa NASA.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

m a p e n z i y a m u n g u 3 6 @ g m a i l . c o m